Na Anastazia Anyimike

# Mifugo, uvuvi vyapunguza umasikini

KATIKA kipindi cha miaka 60 ya uhuru, rasilimali za mifugo na uvuvi zimetoa mchango mkubwa katika maendeleo ya uchumi, kuongeza Pato la Taifa na wananchi, kuondoa umasikini na kuimarisha upatikanaji na usalama wa chakula.

Haya yalisemwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mshimba Ndaki wakati akielezea mafanikio ya sekta ya mifugo na uvuvi nchini tangu Tanzania ilipopata uhuru mwaka 1961.

Alisema wananchi wameendelea kunufaika na rasilimali za mifugo na uvuvi kwa kuongeza kipato, kuondoa umaskini na kuimarisha upatikanaji wa usalama wa chakula.

Aidha, Ndaki alisema ndani ya miaka 60, idadi ya mifugo nchini imeongezeka kutoka milioni 15.4 mwaka 1961 hadi milioni 67.3 mwaka huu.

Alisema ng'ombe wameongezeka kutoka milioni 8, mbuzi milioni 4.4, kondoo milioni 2.99 na nguruwe 22,000 mwaka 1961 hadi ng'ombe milioni 33.9, mbuzi milioni 24.5, kondoo milioni 8.5 na nguruwe milioni 3.2 mwaka jana.

"Mwaka 2021 wapo kuku milioni 87.7 wakiwamo wa asili milioni 40.4 na wa kisasa milioni 47.3," alisema.

Ndaki alisema asilimia 97 ya ng'ombe wanaofugwa nchini ni wa asili na serikali imeongeza matumizi ya mbegu bora kwa njia ya uhimilishaji kutoka uhimilishaji wa ngombe 12,500 mwaka 1961 hadi 77,400 mwaka 2020/21, huku wataalamu wa uhimilishaji 2,700 wakijengewa uwezo.

Kwa upande wa minada, Ndaki alisema mwaka 1961 kulikuwa na minada ya awali 300 ikilinganishwa na minada ya wali 506 mwaka huu, minada ya upili minane na minada ya mpakani minne ikilinganishwa na minada ya upili 18 na minada ya mpakani 13 mwaka huu.

Alisema uzalishaji wa maziwa ulikuwa lita 334,000 mwaka 1961 ikilinganishwa na lita bilioni 3.1 mwaka 2020/2021, huku idadi ya ng'ombe wa maziwa ikiongeka kutoka 198,000 mwaka 1961 hadi milioni 1.2 mwaka huu.

Ndaki alisema usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka wastani wa lita 41,026,000 mwaka 1961 hadi wastani wa lita milioni 75.9 mwaka huu, huku idadi ya viwanda vya kusindika bidhaa hiyo vikiongezeka kutoka saba mwaka 1974 hadi 105 mwaka huu vyenye uwezo wa kusindika wastani wa lita 871,700 kwa siku.

Aidha, alisema uzalishaji wa nyama umeongezeka kutoka tani 97,000 mwaka 1961 hadi tani 738,166 mwaka huu, kati ya hizo, nyama ya ng'ombe ni tani 508,355.17, mbuzi na kondoo tani 102,137.22, nguruwe tani 41,467.82 na kuku tani 86,205.78.

Alisema viwanda vya kusindika nyama navyo vimeongezeka kutoka kimoja mwaka 1961 (Tanganyika Parkers) kilichokuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 800 kwa siku hadi viwanda 11 vyenye uwezo wa kusindika tani 374 kwa siku "Pia kuna machinjio za kisasa 24 zenye uwezo wa kuchinja ngombe 6,360, mbuzi na kondoo 16,050 na kuku 36,500 kwa shifti moja kwa siku mwaka huu zenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 324,800 na mbuzi/kondoo 800,000 kwa mwaka.

Ndaki alisema ongezeko la viwanda vimeongeza upatikanaji wa nyama kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi, ambapo soko la nje ya nchi mwaka 1961 lilikuwa tani 2,150 ikilinganishwa na tani 5,560 mwaka 2020/2021

Alisema pia ukusanyaji wa ngozi umeongezeka kutoka vipande vya ngozi za ng'ombe milioni 1.1, za mbuzi milioni 1.275 na za kondoo milioni 0.4 mwaka 1965 hadi ngozi za ng'ombe milioni 4.17, za mbuzi milioni 5.96 na za kondoo milioni 1.64 mwaka huu.

Aidha, mwaka 1961 jumla ya vipande 1,518 vya ngozi viliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na vipande milioni 1.5 mwaka 2020/21, huku viwanda vikiongezeka kutoka kimoja mwaka 1961 hadi tisa mwaka huu.



1961-2021

MIAKA 60 YA UHURU;
Tanzania imara, Kazi iendelee.

## Magonjwa ya mifugo yadhibitiwa

SERIKALI imepiga hatua katika udhibiti wa magonjwa ya mifungo na kujitegemea katika uzalishaji wa chanjo.

Akizungumza kuhusu mafanikio ya sekta ya mifugo katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru, mjini Dodoma jana, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema kumekuwa na udhibiti wa magonjwa ya mifugo kutokana na kuwa na mfumo endelevu wa uratibu wa udhibiti wa magonjwa hayo kulingana na miongozo ya kitaifa na kimataifa.

Alisema katika kuhakikisha udhibiti wa magonjwa ya mifugo unafanyika kwa ukamilifu, serikali ili tambua magonjwa 13 ya kipaumbele ambapo uwekezaji mkubwa umefanyika kwa kujenga kiwanda cha chanjo cha serikali kinachozalisha chanjo aina sana mwaka huu ikilinganishwa na chanjo 0 mwaka 1961.

Alisema chanjo hizo zinazalishwa kupitia Taasisi ya Kuzalisha Chanjo Tanzania (TVI) ambazo ni za magonjwa ya mdondo wa kuku, kimeta kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo, chambavu kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo, chanjo mchanganyiko ya kimeta na chambavu, ugonjwa wa kutupa mimba kwa ng'ombe, homa ya mapafu ya ng'ombe na homa ya mapafu ya mbuzi.

"Pia chanjo mbili mpya za kichaa cha mbwa na sotoka ya mbuzi na kondoo ziko katika hatua za awali za utengenezaji," alisema.

Ndaki alisema pia kiwanda cha kuzalisha chanjo cha Hester Bioscience mkoani Pwani ujenzi wake umekamalika na uzalishaji wa chanjo za wanyama zaidi ya 27 utaanza hivi karibuni.

Alisema kutokana na juhudi hizo za serikali, kumekuwapo na ongezeko la dozi za chanjo zinazozalishwa nchini kwa mwaka, ambapo mwaka 1961 hakukuwa na chanjo na sasa zimefikia dozi milioni 63.6 sawa na asilimia 6.8 ya mahitaji mwaka 2020/21 ambayo ni jumla ya dozi 936,269,700.

Ndaki alisema pia wametokomeza ugonjwa wa sotoka ambapo kwa sasa Tanzania imepata cheti cha Shirika la Wanyama Ulimwenguni (OIE) cha kuwa huru na maambukizi ya ugonjwa huo.

Alisema katika kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe, serikali ilijenga josho Mpwapwa mwaka 1905 na baada ya uhuru kulikuwa na majosho 707 na kwa sasa kuna majosho 2,763 sawa na ongezeko la asilimia 344.

"Magonjwa yaenezwayo na kupe yamepungua kutoka matukio 1,256 mwaka 1961 hadi matukio 5,985 mwaka 2021," alisema.

Alisema pia ugonjwa wa malale kwa binadamu umepungua kutoka wagonjwa 1,700 mwaka 1991 hadi wagonjwa sita mwaka huu, huku kukiwa na viwanda vinne vya dawa za wanyama.

Aidha, Ndaki alisema idadi ya madaktari wa mifugo waliosajiliwa imeongezeka kutoka 39 mwaka 1961 ambao wote walikuwa ni wageni hadi i 1,061 mwaka huu ambao asilimia zaidi ya 99 ni Watanzania.

## Uvuvi wachangia 1.7% Pato la Taifa



SHUGHULI za uvuvi na maisha ya wavuvi wadogo nchini zimeongezeka katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru, huku sekta hiyo ikichangia Pato la Taifa kwa asilimia 1.7.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (pichani) wakati akielezea mafanikio ya sekta ya mifugo na uvuvi katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru.

Alisema katika kipindi cha mwaka 1961 – 1988 shughuli za uvuvi katika maeneo yote ya uvuvi nchini zilikuwa zikifanywa na wavuvi wadogo huku kiasi cha samaki kilichozalishwa na wavuvi wadogo kutoka kwenye maji asili kimeongezeka kutoka tani 385,771.80 zenye thamani ya Sh bilioni 7.73 mwaka 1986 hadi tani 473,592.24 zenye thamani ya Sh trilioni 2.36 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 18.54.

Ndaki alisema baada ya uhuru, wavuvi wadogo waliendelea kutumia zana duni za uvuvi ambapo takribani asilimia 80 ya vyombo vyote vya uvuvi vilikuwa vikitumia kasia kama nyenzo.

Alisema mwaka 1987, kati vyombo 6,667 vilivyokuwa vikifanya shughuli zake katika Ziwa Victoria, ni 172 vilivyokuwa vikitumia injini za kisasa ikilinganishwa na mwaka 2008 kati ya vyombo vya uvuvi 58,231, vyombo 8,191 vilikuwa vikitumia mashine za kisasa, idadi hii imeendelea kuongezeka hadi kufikia 13,593 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 65.

Alisema kumekuwapo na ongezeko la idadi ya wavuvi, vyombo vya uvuvi na kiasi cha samaki kilichovunwa kuanzia mwaka 1995, ambapo idadi ya wavuvi ilikuwa 75,621, vyombo vya uvuvi 22,976 na kiasi cha tani 255,900.74 za samaki zenye thamani ya Sh 70,467,575.96 zilivunwa ikilinganishwa na idadi ya wavuvi 195,435 waliotumia vyombo 58,231 na kuvuna tani 473,592.24 za samaki zenye thamani ya Sh 2,367,961,211.36 mwaka 2020.

Alisema katika kuimarisha ubora wa mazao ya uvuvi katika mnyororo wa thamani, serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya uvuvi ikiwamo ujenzi na ukarabati wa mialo ya kupokelea samaki na masoko.

Alisema hadi sasa kuna jumla ya mialo ya kisasa 33 na masoko 17 ikilinganishwa na mwaka 1961 ambapo hapakuwa na mialo iliyoboreshwa na masoko ya kisasa.

"Kufuatia juhudi hizo kiasi cha mazao ya uvuvi yanayouzwa nje ya nchi yameendelea kuongezeka kutoka tani 17,269.90 na samaki wa mapambo 4,116 zenye thamani ya Sh bilioni 11.93 mwaka 1995 hadi tani 40,477.97 na samaki wa mapambo 128,316 zenye thamani ya Sh bilioni 386.37 mwaka 2020."

"Aidha, mauzo hayo yaliingizia taifa Sh milioni 629.57 mwaka 1995 ikilinganishwa na Sh bilioni 21.67 mwaka 2020 kama mrahaba," alisema.

Scanned with CamScanner

yani
a
ili-

hususani katika sekta ya nishati vijijini.

Mwenyekiti huyo aliele-

kuwa watatekeleza maagizo yote waliyowapatia.

HABARI LEO UK 16

SQ005066

# Wanaokiuka maadili Mifugo kukiona

**Na Anastazia Anyimike, Dodoma**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki ameagiza kuchukuliwa hatua za kisheria na kinidhamu kwa wataalamu wa afya ya wanyama wakiwemo madaktari wa mifugo ambao wanaenda kinyume na maadili ya taaluma yao.

Ndaki alisema hayo juzi jijini hapa wakati wa kufungua mkutano wa 39 wa kisayansi wa Chama cha Madaktari wa Wanyama Tanzania (TVA) unaofanyika kwa siku tatu.

Alisema baadhi ya wataalamu wa afya ya wanyama na madaktari wa mifugo wamekuwa wakitoa chanjo kwa mifugo kinyume na utaratibu jambo ambalo linasababisha madhara kwa mifugo ikiwemo vifo.

Waziri alisema wajibu wa wataalamu wa afya ya wanyama ni kuhakikisha wafugaji na mifugo wako salama. Alisisitiza kuwa kwenda kinyume kunaongeza changamoto kwa wafugaji.

Aidha, Ndaki alilielekeza Baraza la Veterinari Tanzania ((RVCT) kusaidia kupambana na wanaokwenda kinyume kwa kuendelea kuwasimamia wanachama wao kuwawajibisha inapotokea ukiukwaji wa taaluma na maadili.

Ndaki aliwataka Watanzania wakiwemo wataalamu wa afya ya wanyama na wanachama wa TVA kuhakikisha wanaelewa vizuri na kusimamia Sheria ya Ustawi wa Wanyama ya mwaka 2008 ili kusimamia kikamilifu sekta ya mifugo.

Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia mifugo, Amosy Zephania, alisema wizara inafikiria namna ya kukabiliana na ukiukwaji mkubwa wa kimaadili na kitaaluma kutoka kwa baadhi ya wataalamu hao maeneo mbalimbali nchini.

Alisema wizara imeanza mapitio ya Sera ya Mifugo ya mwaka 2006 iliyodumu zaidi ya miaka 15 huku ikihitaji ushiriki kutoka kwa wafugaji na wataalamu ili kuainisha upungufu uliomo na kuyafanyia marekebisho.wataalamu hao.

Scanned with CamScanner

Profesa Mkenda aliyasema hayo jana katika ziara yake nchini Uganda wakati

hicho kinufaishe wananchi wanaolizunguka.

"Sababu moja ya kuja

HABARI LEO UK 18

# Wasafirishaji samaki walia vikwazo kiwanja cha ndege Mwanza

**Na Suleiman Shagata, Mwanza**

WASAFIRISHAJI wa minofu wa Kanda ya Ziwa wametaka mamlaka zinazohusika na usafirishaji wa anga kuondoa vikwazo vilivyopo kiwanja cha ndege cha Mwanza ili kushawishi wawekezaji kukitumia kiwanja hicho na hivyo kuliingizia pato taifa.

Walitoa ombi hilo jana katika mkutano mkuu wa wadau wa huduma ya usafiri wa anga nchini unaofanyika mjini hapa kujadili namna ya kutumia kiwanja hicho kuleta tija chanya katika uchumi na biashara mkoani Mwanza.

Meneja wa Kiwanda cha kuchakata minofu ya samaki cha Victoria Perch cha jijini Mwanza, Dk Edwin Okong'o alisema wangependa kutumia kiwanja hicho lakini upo ucheleweshaji katika kupakia minofu ya samaki kwenye ndege.

Pia alisema kutokuwepo kwa ndege nyingi za kusafirisha mizigo kwenda katika masoko ya nje ni sababu nyingine zinazofanya watumie kiwanja cha ndege jijini Nairobi, Kenya na Kampala nchini Uganda badala ya Mwanza.

Alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kusafirisha mzigo wa minofu ya samaki uliotosheleza kwenda nchi za nje hivyo aliomba hatua zichukuliwe kurekebisha changamoto hizo mizigo isafirishwe kutoka katika kiwanja hicho kwenye soko la uhitaji wa bidhaa hizo.

Meneja wa Kiwanja cha Ndege Mwanza, Paschael Kalumbete alisema kwa sasa changamoto ya upakiaji wa mizigo imerekebishwa kwani wana uwezo wa kupakia tani mbili hadi nne kwa nusu saa.

Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Hamza Johari aliwahamasisha wafanyabiashara ya minofu ya samaki kutumia kiwanja cha ndege Mwanza akisema kina miundombinu yote muhimu ya kusafirishia minofu ya samaki kwa sasa.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel alisema usafiri wa anga ni kichocheo muhimu kwa kukuza uchumi wa taifa lolote. Alihimiza changamoto zilizopo katika kiwanja hicho zipatiwe ufumbuzi kitumike ipasavyo.

Scanned with CamScanner

TAKUKURU YAAGIZWA KULINDA MASLAHI YA TAIFA NDANI

ISSN 1821-570X
TOLEO NA. 5250
IJUMAA
NOVEMBA 26, 2021
TSH. 1,000
KSH. 100

# HabariLEO

GWIJI LA HABARI TANZANIA

www.habarileo.co.tz

UK7, 16, 18

TANZANIA SENSA 2022 Jiandae Kuhesabiwa



Rais Samia Suluhu Hassan akihutubia mkutano wa 20 wa taasisi za kifedha, Dodoma jana. (Picha na Iddy Mwema).

# Samia ataka uchumi kidijiti

- BoT yasema utakua kwa asilimia nane
- Benki zajiandaa kushusha riba

Uk.2

## BENKI YA DUNIA, WADAU WAPONGEZA WALIOPATA UJAUZITO KURUDI SHULENI

» UK19

## Miaka 60 ya Uhuru:

# Sekta ya mifugo, uvuvi yakua, yapunguza umasikini nchini

Uk.7

1961-2021
MIAKA 60 YA UHURU
Tanzania imara, Kazi iendelee

Toleo Maalumu la
Uhuru

Magazeti ya **DAILY NEWS na HABARILEO** yatachapisha Toleo Maalumu Siku ya tarehe 9 Desemba, 2021 kwa ajili ya Kumbukizi ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Nyote Mnakaribishwa.

Ukitangaza kuanzia nusu ukurasa, unapata nafasi kwenye mitandao ya kijamii na tovuti yenye wasomaji zaidi ya milioni 15.

*Wahi ofa hii kabla ya 05.12. 2021.*

Mawasiliano zaidi:

DAILY NEWS HabariLEO SpotiLEO sundaynews



## MAJALIWA AHIMIZA MADAWATI YA JINSIA SEKONDARI, MSINGI

» UK.3

## SERIKALI YAPATIWA MKOPO BIL 268/- ZA BARABARA

» UK.3

Sensa kwa maendeleo, jiandae kuhesabiwa.

NIPASHE UK 8

# Bandari ya uvuvi sasa kujengwa Kilwa Masoko

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi inaendelea kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi kupitia mtaalamu mwelekezi ambaye ni Kampuni ya M/S Sering Ingegneria ya Italia kwa gharama ya Sh. 1,421,041,703.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alibainisha hayo jana alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio ya sekta ya mifugo na uvuvi kwa waandishi wa habari katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

Alisema serikali tayari imechagua eneo la Kilwa Masoko kwa ajili ya kujenga bandari ya uvuvi.

"Katika mwaka huu wa fedha 2021/2022, serikali imetenga kiasi cha Sh. bilioni 50 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari hiyo mara baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu.

Aidha, alisema jitahada za kutafuta wawekezaji wa kujenga miundombinu mingine ya uvuvi katika eneo hilo zinaendelea vizuri.

Pia, alisema serikali inaendeleza jitihada za kuthibiti ubora na usalama wa samaki na mazao ya uvuvi ili kulinda soko la ndani na nje ya nchi.

Alisema jitihada hizo ni pamoja na kuanzisha Maabara ya Taifa ya Uvuvi Nyegezi mnamo mwaka 1997.

"Ndugu wanahabari, vilevile, katika kuimarisha ubora wa mazao ya uvuvi katika mnyororo wa thamani, serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya uvuvi ikiwamo ujenzi na ukarabati wa mialo ya kupokelea samaki na masoko," alisema Ndaki.

Alisema hadi sasa kuna jumla ya mialo ya kisasa 33 na masoko 17 ikilinganishwa na mwaka 1961 ambapo hapakuwa na mialo iliyoboreshwa na masoko ya kisasa.

Pia, alisema kufuatia juhudi hizo, kiasi cha mazao ya uvuvi yanayouzwa nje ya nchi yameendelea kuongezeka kutoka tani 17,269.90 na samaki wa mapambo 4,116 zenye thamani ya Sh. bilioni 11.93 mwaka 1995 hadi tani 40,477.97 na samaki wa mapambo 128,316 zenye thamani ya Sh. bilioni 386.37 mwaka 2020.

Aidha, alisema mauzo hayo yaliingizia Taifa Sh.milioni 629.57 mwaka 1995 ikilinganishwa na Sh. bilioni 21.67 mwaka 2020 kama mrahaba.

Vilevile, alisema serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia uwekezaji katika sekta ya uvuvi kwa kufanya mapitio ya mara kwa mara ya kuboresha sera, sheria, kanuni na taratibu.

Alisema wizara imeanzisha Dawati la sekta binafsi kwa ajili ya kutoa elimu, kuwaunganisha wadau wa uvuvi na taasisi za kifedha ili kuwawezesha kupata mikopo yenye masharti nafuu.

Alifafanua kuwa kutokana na jitihada hizo, idadi ya viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi imeongezeka kutoka viwanda vinne vilivyokuwa na uwezo wa kuzalisha tani tatu mwaka 1992 hadi 15 vyenye kuzalisha tani 40 hadi 60 kwa siku kwa mwaka 2021.

Hata hivyo, alisema tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya uvuvi katika kina kirefu cha bahari (DSFA) hadi mwaka 2021/2022, jumla ya meli za uvuvi 502 zimepatiwa leseni zenye thamani ya Sh. 24,314,736,449 ambapo jumla ya tani za ujazo 67,437.90 za samaki zilivuliwa katika EEZ ya Tanzania kwa wastani wa tani 6,130.7 kwa mwaka.



Scanned with CamScanner

makazi hayo ulianza kutekelezwa Novemba 22, mwaka huu, jambo lililosababisha

hiyo ili eneo hili haki itendeke, nisisikie fujo kwani mkiendelea litabaki hivyo.

naodaiwa kuwakamata kutokana na kuanzisha vurugu katika eneo hilo na wataka-

hilo akiwamo Salum Hashimu, aliiomba serikali kuwaangalia wakati suala hilo likiendelea.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Dk. Mashimba Ndaki, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, wakati akiwasilisha taarifa ya mafanikio na mwelekeo katika sekta ya mifugo na uvuvi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

pokuwa akifungua tawi la Benki Kuu Mwanza aligusia suala la riba za mikopo na kuzitaka benki zipunguze riba ili sekta binafsi ikope na

wafanye hivyo ili maendeleo yaje kwa haraka zaidi.

Aidha, alisema Serikali inamalizia sera ya mkakati wa kukuza

Naye Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Profesa Florens Luoga alisema kuwa wametekeleza hatua kadhaa

imia 10.

Alitaja hatua nyingine ni kuongeza ukomo wa miamala ya kila siku kwa mteja wa hudu-

ili taasisi hizo ziweze kukopesha sekta ya kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10 kwa mwaka.

MWANANCHI UK 2

# *Bandari ya uvuvi kunufaisha wavuvi 30,000*

Sharon Sauwa, Mwananchi
ssauwa@mwananchi.co.tz

**Dodoma.** Serikali imesema inajenga bandari ya uvuvi wilayani Kilwa Masoko katika Mkoa wa Lindi, huku watu takribani 30,000 wakitarajiwa kunufaika nayo.

Ujenzi wa bandari hiyo ya aina yake hapa nchini unatarajiwa kuanza mwakani.

Akizungumza wakati wa kuelezea mafanikio ya sekta ya mifugo na uvuvi katika miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema wizara inaendelea kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo.

Alisema upembuzi huo unafanywa na mtaalamu mwelekezi ambaye ni kampuni ya M/S Sering Ingegneria ya nchini Italia kwa gharama ya Sh1.42 bilioni.

Alisema katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga kiasi cha Sh50 bilioni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari hiyo mara baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu.

"Tumempa muda awe amekamilisha kazi hiyo ya kufanya upembuzi yakinifu Januari 2022. Akimaliza sisi tutaanza moja kwa moja kutangaza tender (zabuni) ya ujenzi wa bandari ya uvuvi. Tutatangaza moja kwa moja kwasababu michoro na kila kitu vyote vimeshakamilika," alisema.

Alisema hata kazi ya utambuzi wa meli zitakazotia nanga katika bandari hiyo imeshakamilika na kwamba hadi Machi mwakani wanaweza kuwa wameshaanza ujenzi wa bandari hiyo.

Alisema jitahada za kutafuta wawekezaji wa kujenga miundombinu mingine ya uvuvi katika

> "Tumempa muda awe amekamilisha kazi hiyo ya kufanya upembuzi yakinifu Januari 2022. Akimaliza sisi tutaanza moja kwa moja kutangaza tender (zabuni)."
>
> **Mashimba Ndaki- Waziri wa Mifugo na Uvuvi**

eneo hilo zinaendelea vizuri.

Alisema ujenzi wa bandari hiyo katika ukanda wa Pwani utawezesha meli zinazovua kutia nanga kwa lengo la kuhaulisha na kuuza samaki, kutoa takwimu sahihi za mazao ya uvuvi, kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya kuchakata samaki na huduma nyingine.

Alisema pia ujenzi huo utawezesha kuzalisha takriban ajira 30,000 na kuongeza pato kwa jamii.

## Mifugo inayokamatwa

Alipoulizwa kuhusu hatua waliyofikia katika urejeshaji wa ng'ombe baada ya mahakama kuamuru kurejeshwa kwa wafugaji, Ndaki alisema wamewaandikia barua makatibu tawala wa mikoa iliyoathirika na tatizo hilo ya kuwataka wawapelekee orodha ya wafugaji walioshinda kesi lakini hawakurejeshewa mifugo yao.

"Orodha hiyo tunaendelea kuipokea na nyingine tulipokea muda mrefu tumeipeleka kwa Wizara ya Katiba na Sheria, lakini bado tunaendelea kupokea na tutakapopokea yote tutampelekea Waziri Mkuu, ili aweze kuchukua hatua stahiki kwa sababu ndiye aliyeitaka," alisema.

Waziri huyo alisema wameweka muda hadi Desemba 15 mwaka huu kuwa ndio mwisho wa kuzipokea taarifa hizo ili waweze kutengeneza taarifa moja inayowajumuisha wote.

Aliwataka wafugaji waliopotelewa mifugo yao katika mazingira hayo kuwa wavumilivu Serikali inalifanyia kazi jambo hilo.

Maelezo yake yanatokana na malalamiko ya baadhi ya wafugaji ambao mifugo yao imekuwa ikiendelea kushikiliwa na vyombo vya dola hata pale wanapokuwa wameshinda kesi zao.




# Mwanza aviation radar to boost fish sales

From EDWARD QORRO in Mwanza

TANZANIA Civil Aviation Authority (TCAA) Director General, Hamza Johari has exuded confidence on the economic prospects of the civil aviation radar installed at Mwanza airport.

Mr Johari said the radar, which is part of the 67.3bn/- worth of state-of-the-art equipment installed at three other major airports in the country, will boost the export of fish products from the Lake Zone region.

The TCAA boss, who was addressing the 50th National Air Transport Facilitation Committee here yesterday, was optimistic that the radar coupled with the presence of a modern cold room facility will boost the export of fish products to other countries.

"For quite some time fish products from Tanzania made their way to Europe through Entebbe and Jomo Kenyatta Aiports, however the installation of the radar and extension of the airport will see more airplanes land in Mwanza," the TCAA boss explained.

Mr Johari also wondered why countries like Belgium preferred Entebbe and JKIA for Freight on board (FOB) services while Mwanza Aiport had all it takes for such services.

"This explains why we've also, in our midst, players from fish processing industry to reverse the situation," he said.

Mr Johari however challenged the Tanzania Airports Authority (TAA) to hasten expansion of the passengers' lounge at Mwanza airport.

The current capacity of the lounge is 200,000 passengers per year. The demand has however shot to 250,000 in the recent past.

In his remarks, Mwanza Regional Commissioner, Robert Gabriel Luhumbi told players in the aviation sector that Mwanza is a new kid on the block on tourism front, with the presence of the Saanane National Park, Gunzert house and the iconic Bismarck rock.

"Our region has a lot of untapped potential to compete with other regions," he said.



## Mabula directs councils to solve land disputes

From MEDDY MULISA in Bukoba

DEPUTY Minister for Lands, Housing and Human Settlements Development, Dr Angelina Mabula, has directed councils countrywide to solve land disputes in their respective areas without waiting for national leaders.

Equally, she reminded legal land owners to ensure that they pay their annual fees on time.

Deputy Minister Mabula made the remarks